JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MULEBA

Shule ya sekondari Rutabo
S.L.P 174
KAMACHUMU, MULEBA.
Tarehe 30/Machi/2022

Namba za simu
Mkuu wa shule 0754506390 / 0685020792
Makamu Mkuu wa Shule 0766382968
Patron 0767592326
Mtaaluma 0755444576/ 0756061438

Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi……
……
S.L.P……
……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUTABO HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA MKOA WA KAGERA MWAKA 2022/2023

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya…….. Shule ya sekondari Rutabo ipo umbali wa kilometa 52 kusini mwa mji wa Bukoba. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Bukoba mjini nauli ni Tsh 2,500/= hadi mji mdogo Kamachumu.

   Pia, shule ipo kilometa 55 kaskazini mwa mji wa Muleba, kupitia njia hii unashauriwa kutelemkia mji mdogo wa Muhutwe, upande basi dogo - Tsh 1,500/- hadi mji mdogo wa Kamachumu. Ukifika mji mdogo wa Kamchumu panda pikipiki hadi shuleni –Tsh 1,000/=.

   Muhula wa masomo utaanza tarehe iliyotangazwa na serikali. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni katika tarehe zilizopangwa na serikali na si vinginevyo.

2. MAMBO YA KUZINGATIA

2.1. ADA NA MICHANGO YA SHULE

Ada na michango ifuatayo ya shule inabidi ilipwe katika Akaunti ya shule namba 32001200072 jina la akaunti ni **MDC RUTABO SECONDARY SCHOOL CAPITATION ACCOUNT** katika Benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh 70,000/= unaweza kulipa kiasi cha Tsh 35,000/= kwa muhula au kulipa yote kwa mara moja.
b) Shilingi 6,000/=kwa ajili ya kitambulisho na picha
c) Shilingi 20,000/=kwa ajili ya taaluma kwa mwaka
d) Shilingi 30,000/=kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine kwa mwaka.
e) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani kwa mwaka.
f) Shilingi 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule.
g) Shilingi 10,000/= kwa ajiri ya huduma ya kwanza kwa mwaka.
h) Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa).

2.2. SARE YA SHULE:-

a) Suruali mbili za rangi nyeusi tii zenye "turn up" na urefu wa kufunika soksi na kisigino lakini sio kuikanyaga . Ziwe na malinda mawili kila upande na mifuko miwili mbele na mfuko mmoja nyuma, isiwe ndogo ya kubana (MODO)
b) Mashati mawili meupe pee ya mikono mirefu na mfuko mmoja upande wa kushoto. Yawe na vishikizo visivyo vya kuchomoa na kuchomeka.
c) Sare za michezo kwa shule hii ni Bukta ya bluu (aje nayo) na Tisheti yenye nembo ya shule inapatikana shuleni Tsh 8,000/- na raba za michezo jozi moja (aje nazo).
d) Mkanda mweusi wa ngozi upana usiozidi inchi mbili na usiwe na picha za watu au wanyama.
e) Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi na visiwe na kisigino kirefu na soksi nyeusi tii, jozi mbili.
f) Sweta rangi ya bluu yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/=
g) Nguo za kushindia (shamba dress) ni: tisheti yenye kola yenye nembo ya shule -Tsh 15,000/=, na " track suit" yenye nembo ya shule Tsh 22,000/=). (vyote utavipata shuleni kwa gharama zilizooneshwa). Viatu vya kushindia vya ngozi "open shoes" rangi nyeusi (aje navyo).
h) Tai ya bluu yenye michilizi nyeupe inapatikana shuleni Tsh 5,000/=

NB. Mavazi yote tofauti na sare zilizobainiswa hapo juu hayaruhusiwi shuleni kabisa.

2.3. MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA

(a) Rimu moja ya karatasi A4 kwa muhula, rimu mbili kwa mwaka. Madaftari. makubwa (Quire 3 au 4) 7 au zaidi. Folder file cover moja. Mathematical set, rula moja na kalamu za kutosha (vinapatikana kweye duka la shule au aje navyo).
(b) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kwa maelezo zaidi wasiliana na mkuu wa shule au mtaaluma. Pia, nakala ya orodha ya majina ya vitabu imeambatanishwa.
(c) Scientific calculator ambayo ni non programmable kwa tahasusi za HGL & HGK.
(d) Godoro ft 2.5 kwa 6 (Unaweza kulipata shuleni kwa bei nafuu)

(e) Mashuka jozi 2 rangi ya pinki ,blanketi 1, mto na foronya - rangi ya pinki, chandarua. (Unaweza kuvipata madukani karibu na shule kwa bei nafuu)
(f) Vyombo vya chakula (sahani ,bakuli ,kijiko, na kikombe) pia unaweza kuvipata kwenye duka la shule. Aje na chupa ya chai ya vikombe 4.
(g) Ndoo mbili kubwa zenye mifuniko.
(h) Kwanja 1 (kwa tahasusi ya HGL), Kotama 2 (kwa tahasusi za HKL & HGK)
(l) Jembe 1, mifagio ya ndani na nje (mopa 1,soft bloom 1 na mifagio ya nje aina ya chelewa 2) kwa tahasusi zote.
(m) Tochi ya betri/Solata
(n) Toilet paper -20 (kila muhula 10) ni lazima kwa matumizi binafsi.
(o) Dawa ya chooni yenye ubora lita 5 kwa mwaka.
(p) Aje na sanduku imara la chuma kwa ajili ya kutunzia mali zake na begi la kubebea madaftari.
(q) Mwanafunzi anashauriwa kuwa na mwamvuli imara mdogo ambao ni rahisi kuutunza.

NB. Kila mwanafunzi aje na nyaraka muhimu zifuatazo:

- **Passport size mbili (zipigwe akiwa amevaa shati jeupe)**
- **Nakala mbili za results slip (CSEE 2021)**
- **Nakala mbili za cheti cha kuzaliwa (birth certificate)**
- **Fomu zote tatu zilizoambatanishwa zikiwa zimejazwa kikamilifu.**

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,waalimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
(vi) Kuwa na mtindo wa nywele usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wanapokua shuleni. (vii) Kufuga ndevu.
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa, sambamba na kukutwa na mpira (kodomu)
(xi) Kumpa binti mimba.
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiv) Kutembea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi, laini ya simu, redio na spika za masikioni (ear phones) katika mazingira ya shule. Simu ya shule kwa ajili ya mawasiliano ya wanafunzi na wazazi au walezi wao ipo: Namba 0762550067
(xvi) Kudharau bendera ya taifa
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k (xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
(xviii) Kukusanyika/kuitisha mkutano bila kibali.

4. SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kutii sheria za shule, walimu, wafanyakazi, viranja na viongozi wote wanaohusika. Ni lazima kila mwanafunzi kufuata taratibu zilizowekwa na vilevile kuwa na tabia nzuri.Mwanafunzi mwenye tabia mbaya na asiye na nidhamu hafai kupewa nafasi ya elimu ya juu.

SHERIA ZA SHULE

a) Kila mwanafunzi awahi shughuli zote kwa wakati unaotakiwa. Kuchelewa kwa aina yoyote bila sababu ni kosa kubwa
b) Vifaa hatarishi kama vile visu, mapanga, majembe, fyekeo, kotama, viberiti, pasi za umeme n.k havitakiwi kabisa kuonekana mabwenini na sehemu nyinginezo shuleni bila sababu maalum.
c) Hakuna mwanafunzi atakayeenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa. Ruhusa ya kutoka nje itatolewa na mwalimu wa zamu kwa maandishi juu ya cheti cha 'PASS'.
d) Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule au makamu wake.
e) Hakuna mwanafunzi atayetoka nje ya mipaka ya shule akiwa na kifurushi au begi bila kibali.
f) Sare za shule(uniform) zivaliwe wakati wote, madarasani au nje ya madarasa.
g) Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalimu au mfanyakazi bila
ruhusa ya mkuu wa shule au makamu wake.
h) Usafi wa mwili na mavazi, madarasani, mabwenini, viwanja na sehemu zote ni wajibu wa kila mmoja. Takataka zisitupwe ovyo.
i) Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali ya shule. Ni kosa kubwa kuharibu
j) mali ya shule hata ikiwa ni ndogo namna gani. Taa na maji lazima vitumiwe kwa
k) uangalifu.
l) Ugomvi, hila, matusi yoyote ya kusoma au kuandika yanakatazwa kabisa.
m) Magazeti au vitabu vyenye picha au maneno yasiyofaa hayaruhusiwi shuleni.
n) Tabia njema ndani na nje ya shule ni wajibu kwa kila mwanafunzi.
o) Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuandika barua ya kiofisi mahali popote nje ya shule bila kuipitisha kwa mkuu wa shule.
p) Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono kama vile anavyoheshimu masomo yake.

q) Ujeuri au ubishi wa aina yoyote kwa walimu, wafanyakazi na viranja ni mwiko.
r) Matatizo yakitokea ajulishwe mwalimu wa bweni, mwalimu wa darasa mwalimu wa zamu au mlezi wa sehemu husika.
s) **Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni**

jambo la lazima.

q) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi.

4.2. MADARASANI

a. Kila mwanafunzi anatakiwa kukaa darasanikatika nafasi yake kwa mpango uliowekwa
b. Wanafunzi lazima wasimame na mwalimu anapoingia na anapotoka darasani.
c. Mwanafunzi haruhusiwi kukalia viti vya walimu.
d. Darasa litasafishwa kila siku asubuhi kufuatia utaratibu uliowekwa na kiranja wa darasa.
a. Ni marufuku kupiga kelele madarasani.
b. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria masomo ipasavyo shuleni na darasani. Asipofanya hivyo kwa kipindi kuanzia siku tisini(90) mfululizo atakuwa amejifuta mwenyewe.

4.3. KAZI ZA NJE

a. Kazi zote za nje zifanywe kwa juhudi na maarifa.
b. Zana/vifaa vya kazi lazima virudishwe vilipotolewa mara baada ya kazi.
c. Yeyote atakayepoteza kifaa atanunua kifaa hicho.
d. Kila mwanafunzi atapewa eneo lake la usafi na alitunze kila siku.

4.4 MABWENI

a. Mwanafunzi haruhusiwi kuwasha moto au kupika.
b. Kila mwanafunzi sharti atandike kitanda chake vizuri anapoamka.
c. Ni marufuku kulala bweni wakati wa kazi au masomo bila kibali.
d. Vyoo vyote vitumike vizuri na kuwekwa katika hali ya usafi wakati wote.

4.5 UKUMBI WA MAAKULI

a. Hakuna mwanafunzi atayeingia jikoni bila kibali.
b. Chakula kitaliwa bwaloni na kamwe kisipelekwe bwenini.
c. Usafi wa bwaloni uzingatiwe wakati wa ugawaji wa mlo na baada ya mlo.
d. Kila mwanafunzzi afuate mpangilio uliowekwa kwa matumizi ya bwalo la chakula. Kelele haziruhusiwi wakati wa mlo.

4.6 ADHABU

1. Walimu na viranja wanaweza kumuadhibu mwanafunzi yeyote anayevunja sheria za shule au taratibu zilizobainishwa.
2. Adhabu inapotolewa itimizwe kwanza kabla ya kupeleka malalamiko mbele.
3. Adhabu itatolewa kulingana na uzito wa kosa na uwezo wa kuitekeleza.
4. Kwa makosa makubwa, mwanafunzi ataadhibiwa na mkuu wa shule mfano, kumsimamisha shule mwanafunzi au kumfukuza kabisa shule.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya mkuu wa shule.....

Jina la mkuu wa shuile: **MUJUNI J. LWENTEME**

Mhuri wa mkuu wa shule.....

HEADMASTER
RUTABO SEC. SCHOOL
BOX 174 KAMACHUMU
MULEBA

SHULE YA SEKONDARI RUTABO

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi.....
(jaza ilivyo kwenye TSM9/SEL FORM)
2. Anwani ya nyumbani.....
3. Tarehe ya kuzaliwa.....mahali ulipozaliwa.....
Mahali unapoishi nyumbani kwenu) Wilaya.....Tarafa.....
Kata.....kijiji.....
4. Shule ya sekondari ulikotoka.....
Anwani..... .....
5. Dini.....
6. Kabila.....
7. Taifa (Mtanzania/Si Mtanzania).....
8. Jamaa katika familia yako:

a) Jina la baba.....
Anwani.....
Anaishi/Haishi.....kazi yake.....
Namba yake ya simu.....

b) Jina la mama.....
Anwani.....
Anaishi/haishi.....kazi yake.....
Namba yake ya simu.....

c) Jina la mlezi.....
Anwani.....
Kazi yake.....namba yake ya simu.....
Uhusiano na wewe.....

Mimi ..... (mwanafunzi) nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli.

Sahihi ya mwanafunzi.....tarehe.....

Mimi .....mzazi/mlezi wa mwanafunzi. ..... nimehakikisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli.

Sahihi ya mzazi/mlezi.....tarehe.....

UONGOZI WA KIJIJI.

Jina la mtendaji wa kijiji.....sahihi.....

Anwani ya mtendaji wa kijiji.....namba ya simu.....

Muhuri.....

.....

FOMU YA MWANAFUNZI KUKUBALI NAFASI NA KUTII SHERIA ZA SHULE, KUTOSHIRIKI MGOMO, FUJO NA MAKOSA YOYOTE YA JINAI

ANWANI.....
.....

Mkuu wa shule,
Shule ya Sekondari Rutabo,
S.L.P 174,
KAMACHUMU.

Mimi..... (Jina la mwanafunzi)
Nimepokea barua ya kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari Rutabo kwa mwaka ..... Nakubali nafasi hiyo kwa moyo mkunjufu, ninahaidi kutoshiriki mgomo, fujo na makosa yoyote ya jinai na kufuata sheria zote za shule. Endapo nitashindwa kutii sheria na maelezo hayo hatua inayostahili ichukuliwe juu yangu. Natoa ahadi hii mbele ya mzazi wangu ambaye ametia sahihi yake hapa chini.

....
Sahihi ya mwanafunzi. Tarehe.

Mimi.....(jina la mzazi)
Ambaye ni mzazi wa ..... nakubali kuwa mtoto wangu ajiunge na shule ya sekondari Rutabo, atii sheria na maelezo kama alivyoahidi mbele yangu. Nitakuwa tayari kushirikiana na watumishi shuleni kwa malezi bora yanayolingana na sheria hizo, sambamba na kulipa ada na michango yote ya shule kwa wakati. Pia niko tayari kupokea na kufanyia kazi maelekezo yote yatakayotolewa shuleni.
Pakiwepo na tatizo ninaweza kuwakilishwa na wafuatao ambao picha zao zimeambatanishwa hapa chini.

S/N	JINA	MAHALI ANAPOISHI	UHUSIANO	NAMBA YA SIMU
1.				
2.				
3.				
4.				

Picha za wahusika hapo juu ni hizi zifuatazo;

1. 2. 3. 4.

Jina la mzazi.....sahihi.....

Namba ya simu.....tarehe.....

UONGOZI WA KIJIJI

Jina la afisa Mtendaji.....

Sahihi.....Namba ya simu.....

Anwani ya afisa mtendaji wa kijiji.....

Muhuri.....

MULEBA DISTRICT COUNCIL

RUTABO SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a medical officer)

Student's Name.....

Age.....

Blood examinatfion: Hemoglobin.....

Any abnormalmalities notes.....

Stool examination.....

Urinalysis.....

T.B test (If negative immunization given).....

.....

Eyes.....

Chest.....

Any chronic complaints not noted above e.g.

Asthma.....

Headache.....

Skin diseases etc.....

Also anything else that the school health staff should know about

.....

Any treatment or recommendation.....

In case of Bilharzias it is recommended that student attend Bilharzias clinic before they come to school.....

.....

I certify that I have examined the above student and recommended that she/he is fit/unfit to pursue secondary education.

Signature of Examiner.....

Date.....

Destination.....

Offici
al stamp.....

ORODHA YA VITABU KWA AJILI YA MASOMO

GEOGRAPHY	1. *Pritchard M, John (1971)* Practical Geography for Africa. 2. *PT. Msabila (2007)* A Comprensive Approach to Physical Geography for Secondary Schools. 3. *Msabila, DT (2000)* An Intergrated Focal Regional Study on Human and Economic Geography. 4. Zist Kamili - Geography new editions for paper 1 and 2
KISWAHILI: A. USHAIRI	***Nunua vitabu vitatu kutoka kila sehemu (A, B & C)*** 1. Haji, G, H. (1994). *Kimbunga*; Dar es Salaam. TUKI 2. Khatibu, M (1988). *Fungate ya Uhuru*;Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press. 3. Mvungi, (1985). *Chungu Tamu*; Dar es Salaam. Tanzania Publishing House. 4. H. J. Mwansoko *Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na Isimu* 5. Rboert S. (1970); *Mapenzi Bora,* Dsm; Evance & Brothers LTD
B. TAMTHILIYA	1. Hussein , E. (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim*;Nairobi Oxford University Press. 2. Mbogo, E (1993). *Morani* ; Dar es Slaam. Dar es Salaam University Press 3. Mohamed, S. A (1990). *Kivuli Kinaishi*;Nairobi Oxford Univestriy Press 4. Penina Mhando; *Nguzo Mama*
C. RIWAYA	1. Msokile, M (1990). *Usiku Utakapokwisha*; Dar es Salaam: Dar es Salaam Univesity Press. 2. Robert, S (1967). *Kufikirika;* Nairobi Oxford Univesity Press 3. Shafi, A.S. (1997). *Vuta n'Kuvute*; Dar es Salam. Oxford University Press. 4. Tuwa, H (2007). *Mfadhili;* Dar es Slaam. Macmillan.
LITERATURE A. NOVELS	***Please select three books from A & B; Two from C (Poems)*** 1. Arm, A.K . (1969). *The Beautiful Ones Are Not Born*; New York: Colllier Macmillan. 2. Chinua, A. (1988). *A Man of the People,* Oxford: Heinemann Education Publishers. 3. Chinua, A. et al. (2000). *Encounters from Africa*. Nairobi. Macmillan Publishers Ltd. 4. Safo, D (1983). *His Excelence The Head of State.* Dar es Salaam. Macmillan. 5. Ndunguru, S. N. (1999). *Divine Providence* . Dar es Salaam; Mkuki na Nyota Publishers.
B. PLAYS C:	1. Ibsen, H (1967). *An Enemy of the People* Nairobi. Heinemen Education Books Ltd. 2. Imbuga, F (1976). *Betrayal in The city* . 3. Ngungi wa Thiong'o & Ngungi wa Mirii, (1982). *I will Marry When I want.* Nairobi 4. Omtatah, O. (2006). *Lwanda Magere*. Dar es Salaam. Mkuki na Nyota Publishers. 5. Bukenya, A (2004). Rugan. J (2005). *Black Mamba*. Dar es Salaam. Mkuki na Nyota Publishers. 6. *The Bridge* . Dar es Salaam. Mkuki na Nyota Publishers.
POEMS	1. Mloka, C (2005). *The Wonderful Surgeon and other Poems* . Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers 2. Tanzania Institute of Education. (1996). *Selected Poems* . Dar Salaam. Tanzania Institute of Education.

ENGLISH ONE: -

1. ADVANCED ENGLISH LANGUAGE FORM 5 AND 6
By Nicholaus Asheli, By Oxford, BY Kadeghe, BY Norbet

2.

2. *English for Form Five and Six*: Phology stylistics and Semantics : By Dr Kadeghe Michael

HISTORY	1. How Europe underdeveloped aaAfrica - By Walter Rodney 2. General History of Africa - By AssaOkot -HISTORY PAPER II ALIVE 3 SALEH YASINHISTORY 1 AND 2 4. Contemporary Historical Events - Vol. I & II By Shibitali C. K Tumaini 5. Mastering Modern World History. - By Norman Lowe
G/STUDIES	1. General Studies For Secondary School - By Mbalase, R. 2. General Studies By SETA 2 GENERAL STUDIES NOTES 3. GENERAL STUDIES SUPPLEMENTARY BOOK FOR A-LEVEL